

*Kioo cha Lughha, Juz. 19(2), 2021, 123-136*

*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*

*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

## **Athari za Irabundefu kwenye Maana na Uainishaji wa Maneno yenye Jozi Pambanuzi Finyu katika Lughya ya Kiswahili: Mifano kutoka Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2013)**

*Elishafati J. Ndumiwe<sup>1</sup>*

### **Ikisiri**

Katika lughya ya Kiswahili aina za maneno na maana katika baadhi ya maneno yenye jozi pambanuzi finyu hutofautiana. Utuftu huo unahusishwa na kuwapo kwa irabundefu katika mojawapo ya jozi ya maneno hayo. Kwa hiyo, makala hii inafafanua athari za irabundefu kwenye maana na uainishaji wa maneno yenye jozi pambanuzi finyu katika lughya ya Kiswahili. Data ya makala hii imekusanywa kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ya mwaka 2013 kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka. Aidha, uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Konsonanti-Irabu ya Clements na Keyser (1983). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba kuwapo kwa irabundefu kunaweza kubadilisha nomino kuwa kitende, kitende kuwa nomino, kiunganishi kuwa nomino na hata nomino kuwa kivumishi au kibainishi. Vilevile, irabundefu huweza kutofautisha maana katika maneno yenye jozi pambanuzi finyu. Pia, utafiti huu unapendekeza kufanyika kwa tafiti ili kubaini sababu ya utuftu wa maana na kategoria katika maneno ya jozi pambanuzi finyu yenye irabufupi.

### **1.0 Utangulizi**

Irabu ni sauti ambayo hutamkwa bila kuwapo kwa kizuizi chochote cha hewa itokayo mapafuni kwenda nje kuitia chemba ya pua na kinywa (Kihore na wenzake, 2012). Kwa kuzingatia kigezo cha wakaa<sup>2</sup>, irabu za lughya ya Kiswahili huainishwa katika makundi mawili: irabundefu na irabufupi (Ndumiwe, 2019). Irabundefu ni irabu ambayo huchukua wakaa mrefu zaidi katika kutamkwa kwake (Massamba, 2016). Aidha, Kiraka (2013) anasititiza kuwa irabu itachukuliwa kuwa na wakaa mrefu ikiwa itakuwa na uzito wa angalau mora<sup>3</sup> mbili katika kutamkwa kwake. Baadhi ya wanaisimu wa lughya ya Kiswahili wamebainisha irabundefu katika lughya ya Kiswahili ambazo ni </a:/, /e:/, /i:/, /ɔ:/ na /u:/> (Choge, 2009; Kiraka, 2013;

<sup>1</sup> Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kiswahili, Kitivo cha Elimu, Chuo Kikuu cha Mt. Agustino Tanzania, Mwanza, Tanzania. Baruapepe: ndumiweelisha@gmail.com

<sup>2</sup> Wakaa ni jumla ya muda unaotumika kutamka sauti au silabi fulani (Massamba, 2016).

<sup>3</sup> Mora ni kipimo cha wakaa wa sauti katika silabi, hasa katika Nadharia ya Fonolojia Mizani (Massamba, 2016).

Mashauri, 2018 na Ndumiwe, 2019). Nayo, irabufupi ni irabu ambayo huchukua wakaa mfupi au wa kawaida katika kutamkwa kwake. Irabu hizo ni </a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/ na /u/> (Kihore na wenzake, 2012).

Hata hivyo, ipo mitazamo miwili tofautitofauti kuhusu utokeaji wa irabundefu katika lugha ya Kiswahili. Mtazamo wa kwanza, irabundefu hutokea baada ya michakato ya kifonolojia. Kuhusu hilo, Kimizi (2003) anasisitiza kuwa irabundefu katika lugha ya Kiswahili hutokana na michakato ya kifonolojia, kama vile urefushaji wa irabu au kuungana kwa irabu katika mipaka ya mofu. Hii ndiyo Massamba (2016) anayoichukulia kama iraburefushwa na anaieleza kuwa hapo mwanzo ilikuwa fupi lakini inalazimika kurefushwa kutokana na kutokea katika mazingira yenyenye mabadiliko ya kifonolojia.

Mtazamo wa pili unaona kuwa irabundefu hutokea kiasilia. Kuhusu hilo, Kimizi (2003) anaeleza kuwa wakati mwingine irabundefu huweza kutokea kiasilia katika mizizi ya maneno (kama <ndogo> → [ndɔ:gɔ] pasipo michakato ya kifonolojia. Hii ndiyo Massamba (2016) anayoichukulia kuwa ni irabundefu na huchukua wakaa mrefu pindi inapotamkwa. Katika kuzitofautisha irabu hizo, Massamba (2016) anaeleza kuwa irabundefu hutokea kwa asili yake ilhali iraburefushwa ni irabufupi kwa asili yake lakini huongezewa wakaa tu katika mazingira maalumu ya kifonolojia. Hata hivyo, Kiraka (2013) anaziita kuwa zote ni irabundefu ijapokuwa zipo zinazotokea kiasilia na nyingine zinazotokana na michakato ya kifonolojia.

Makala hii inaafikiana na mtazamo wa Kiraka (2013) kwa kutumia istilahi ya irabundefu kwa sababu irabu ikirefushwa huwa na uzito wa mora mbili bila kuzingatia kuwa imetokea kiasilia au baada ya michakato ya kifonolojia. Zaidi ya hayo, tofauti ya nyakaa kati ya irabu zinazorefushwa na zenye urefu kwa asili katika maneno ni ndogo mno kiasi kwamba nyakaa hizo hufanana. Aidha, ieleweke kuwa wakaa ndiyo husababisha irabu kuwa fupi au ndefu. Kwa hiyo, irabu huwa fupi ikiwa ina wakaa unaotumika kutamka irabu hiyo ni mfupi ilhali irabu huwa ndefu ikiwa wakaa unaotumika kutamka irabu hiyo ni mrefu.

Aidha, irabundefu katika lugha ya Kiswahili zina mazingira maalumu ya kutokea kwake. Kiraka (2013) anadokeza kuwa panaelekeea kuwa na ruwaza mbalimbali za utokeaji wa irabundefu katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, irabundefu katika lugha ya Kiswahili hutokea katika mazingira tofautitofauti. Kwanza, irabundefu hutokea kabla ya mfuatano wa nazali na konsonanti nyinginezo. Baadhi ya wanaisimu wa lugha ya Kiswahili wanaeleza kuwa lugha hii ina utaratibu wa kurefusha irabu zinazotokea kabla ya mfuatano wa nazali na konsonanti nyinginezo (Polome, 1967; Hyman, 2003). Aidha, Massamba (2005) anasisitiza kuwa irabu inayotokea kabla ya mkururo wa nazali na konsonanti nyingine (iliyopo katika silabi moja) ni ndefu aghalabu si irabu inayorefushwa. Kwa maana hiyo,

irabundefu katika mazingira haya hutokea kiasilia. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya:

1. (a) skonzi ['skɔ:nzi]  
 (b) shamba ['ʃa:mba]  
 (c) ponza ['pɔ:nza]  
 (d) mpunga [mu'pu:nga]  
 (e) shangazi [ʃa:'ngazi]
- Chanzo:** TUKI (2013)

Katika mifano 1 (a)-(e) irabu zilizopo kabla ya mkururo wa nazali na konsonanti nyinginezo hutokea kama irabundefu pasi kupidia mchakato wowote wa urefushaji. Aidha, imebainika kuwa ili irabu iwe ndefu kwa mazingira ya namna hii, sharti mkururo wa nazali na konsonanti nyingine utokee kuanzia silabi ya pili na kuendelea wala si katika silabi ya kwanza. Katika mazingira ya namna hiyo tunaweza kupata utokeaji wa irabundefu kwa asilia.

Pili, irabundefu hutokea katika silabi yenyе mkazo msingi, yaani silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno. Hyman (2003) anathibitisha hilo kwa kueleza kuwa lugha za Kibantu za Mashariki na Kusini hurefusha irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho. Aidha, Mashauri (2018) anaeleza kuwa mara nyingi irabu yenyе mkazo msingi katika lugha ya Kiswahili hutamkwa kwa wakaa mrefu kuliko irabu nyinginezo katika neno hilo. Mifano katika 2 (a)-(e) inaweza kurejelewa ili kudhihirisha haya.

2. (a) stesheni [ste'ʃe:ni]  
 (b) pamba ['pa:mba]  
 (c) rimoti [ri'mɔ:ti]  
 (d) songombingo [sɔŋɔ'mbi:ngɔ]  
 (e) sukuma [su'ku:ma]
- Chanzo:** TUKI (2013)

Tukirejea mifano 2 (a)-(e) tunabaini kuwa irabundefu hutokea katika silabi ya pili kutoka mwisho ambayo mara nyingi hubeba mkazo msingi katika maneno hayo. Aidha, Kimizi (2003) anasisitiza kuwa utokeaji wa irabundefu katika silabi yenyе mkazo msingi hutokea kiasilia bila kuhusishwa kwa mchakato wa kifonolojia.

Mwisho, irabundefu hutokea katika maneno yenyе mkururo wa konsonanti halisi. Muundo wa silabi katika lugha za Kibantu, Kiswahili kikiwamo, hauruhusu mfuatano wa konsonanti halisi, mfuatano wa konsonanti usiohusisha viyeyusho. Maneno yenyе mkururo wa konsonanti halisi katika lugha za Kibantu yametokana na athari kutoka lugha za kigeni hasa Kiingereza na Kiarabu (Massamba, 2011; Ndumiwe, 2019). Hivyo basi, irabu zinazotokea kabla au baada ya mkururo wa konsonanti halisi huelekea kuwa ndefu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

3. (a) brashi ['bra:fɪ]  
 (b) drafti ['dra:fɪ]  
 (c) padri ['pa:dɪ]  
 (d) kabla ['ka:bla]  
 (e) nakshi ['na:kʃɪ]

**Chanzo:** TUKI (2013)

Katika mfano 3 (a) irabundefu hutokea baada ya mkururo wa konsonanti halisi. Aidha, katika mifano 3 (c)-(e) irabundefu imetokea kabla ya mkururo wa konsonanti halisi. Hata hivyo, katika mfano 3 (b) irabundefu imetokea kabla na baada ya mkururo wa konsonanti halisi. Utokeaji wa irabundefu katika mkururo wa konsonanti halisi unahusishwa na mambo mawili. Mosi, mwangwi wa matamshi ya irabundefu au irabuunganifu kutoka lugha chanzi hasa Kiingereza au Kiarabu. Pili, ufidiaji wa irabu iliyopotea baada ya mkururo konsonanti halisi kwa sababu lugha ya Kiswahili kiasilia haina mkururo wa namna hiyo. Kwa hiyo, utokeaji wa irabundefu katika mazingira haya hauhusishwi na sababu moja rasmi.

Kwa ujumla, urefushaji wa irabu siyo sifa inayojipambanua katika maandishi bali katika matamshi. Ni vigumu kuhitimisha kuwa kila neno la Kiswahili lina irabundefu au la katika mojawapo ya silabi zake bali utafiti zaidi unahitajika katika kipengele hiki. Hata hivyo, kuna maneno yana irabupacha ambazo siyo irabundefu. Maneno haya yana irabupacha zinazofuatana katika neno hilohilo huku kila irabu ikiwa katika silabi yake. Mara nyingi, irabu ya kwanza ni kilele cha silabi iliyotangulia na irabu ya pili ni mwanzo wa silabi inayofuata (Stegen, 2005). Kwa mfano, katika neno “muuguzi” [\$mu\$\$u\$\$gu\$\$zi\$] silabi ya pili kutoka mwanzoni \$u\$ hutamkwa kivyake wala si mwendelezo wa irabu /-u-/ ya silabi ya kwanza \$mu\$. Makala hii imegawanyika katika sehemu tano: utangulizi, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data, athari ya irabundefu kwenye uainishaji wa maneno yenye jozi pambanuzi finyu, athari ya irabundefu kwenye maana za maneno yenye jozi pambanuzi finyu katika lugha ya Kiswahili na hitimisho.

## 2.0 Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data

Data za makala hii zimekusanywa kutoka katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2013) kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, toleo la 3 (KKS 3, kuanzia sasa) imeteuliwa kwa sababu maneno yenye jozi pambanuzi finyu<sup>4</sup> yameingizwa kama vidahizo. Mwandishi wa makala hii aliteua homonimu<sup>5</sup> na vidahizo vingine kutoka kamusi teule ili kuchunguza ikiwa utofauti wa maana na kategoria katika vidahizo hivyo unatokana na kuwapo kwa irabufupi, irabundefu au la. Hata hivyo, katika KKS 3 vidahizo hivyo havina irabundefu katika mojawapo ya

<sup>4</sup> Maneno yenye jozi pambanuzi finyu ni maneno yenye fonimu zinazofanana lakini yanatofautiana katika sifa za kifonetiki kidogo sana (Massamba, 2016).

<sup>5</sup> Homonimu ni mojawapo ya maneno mawili au zaidi yenye umbo moja lakini yenye maana tofauti (Massamba, 2016).

jozi moja. Kwa hiyo, mtafiti aliwateua wazungumzaji 5 wa lugha ya Kiswahili kutoka kata ya Nyegezi, wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza kwa mbinu ya usampulishaji lengwa ili watunge sentensi moja kwa kila kidahizo kwa kuzingatia jozi pambanuzi finyu. Baada ya wazungumzaji hao kutunga sentensi, mtafiti alibaini kuwa utofauti wa maana na aina katika baadhi ya maneno yenye jozi pambanuzi finyu husababishwa na kuwapo kwa irabundefu katika mojawapo ya jozi ya maneno hayo.

Aidha, uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Konsonanti-Irabu (Nadharia ya KI, kuanzia sasa) ya Clements na Keyser (1983). Nadharia hii inahusu uwakilishi wa silabi katika neno. Kwa mujibu wa Nadharia ya KI, fundo-mama pamoja na vifundo-dada hugawika kiuwili. Fundo-mama huwakilisha ngazi ya juu ya silabi na vifundo-dada huwa ni mwanzo na kilele cha silabi. Fundo-dada la kushoto ndiyo mwanzosilabi na mara nyingi hukaliwa na konsonanti. Aidha, fundo-dada la kulia huwa ni upeosilabi na mara nyingi hukaliwa na irabu. Wakati mwingine, irabu pekee inaweza kuwa mwanzosilabi na upeosilabi. Kwa hiyo, Nadharia ya KI imetumika kuchanganua fundo-dada la kushoto ambalo ni upeosilabi kuona kama ina sifa ya kutofautisha maana na kubadili kategoria katika maneno yenye jozi pambanuzi finyu ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, irabundefu hupatikana katika fundo-dada la kushoto.

### **3.0 Athari za Irabundefu katika Uainishaji wa Maneno ya Kiswahili**

Uainishaji wa maneno ya Kiswahili huzingatia mofolojia ya neno au uamilifu wa neno hilo katika sentensi (Mgullu, 1999). Kwa mfano, neno linakuwa kitenzi kwa sababu linataja tendo linalofanyika, litakalofanyika au lililofanyika. Aidha, neno linakuwa nomino kwa sababu linataja jina. Hata hivyo, baadhi ya maneno huamuliwa na matamshi ili kuyaingiza katika kategoria fulani. Matamshi hayo yanahusishwa kuwapo kwa irabundefu na irabufupi katika maneno hayo. Hii ina maana kwamba neno likiwa na irabufupi huwa la kategoria fulani lakini likiwa na irabundefu kategoria ya neno hilo hubadilika. Kwa hiyo, katika sehemu hii tumepambanua athari za utokeaji wa irabundefu katika uainishaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umebaini kwamba irabundefu huathiri uainishaji wa maneno yenye jozi pambanuzi finyu kama inavyothibitika katika vipengele vifuatavyo:


#### **3.1 Ubadilikaji wa Kitenzi kuwa Nomino**

Makala hii imebaini kuwa baadhi ya maneno yakiwa na irabufupi huwa ni vitenzi lakini yakiwa na irabundefu katika mazingira hayohayo hubadilika kuwa nomino. KKS ya 2013 imefanikiwa kuonesha kuwa baadhi ya maneno yenye jozi pambanuzi finyu yapo katika kategoria tofauti. Hata hivyo, utofauti huu haukuhusishwa na utokeaji wa irabundefu katika mojawapo ya jozi ya maneno hayo. Mifano 4 (a)-(f) na 5 (a)-(f) inadhihirisha haya.

- |    |                        |    |                         |
|----|------------------------|----|-------------------------|
| 4. | (a) tupa ['tupa] (T)   | 5. | (a) tupa [t'u:pa] (N)   |
|    | (b) chuma ['ʃuma] (T)  |    | (b) chuma ['ʃu:ma] (N)  |
|    | (c) wana ['wana] (t)   |    | (c) wana ['wa:na] (N)   |
|    | (d) kiko ['kikɔ] (T)   |    | (d) kiko ['ki:kɔ] (N)   |
|    | (e) shuka ['ʃuka] (T)  |    | (e) shuka ['ʃu:ka] (N)  |
|    | (f) tenda ['tenda] (T) |    | (f) tenda ['tɛ:nda] (N) |

Chanzo: TUKI (2013)

Maneno katika mifano 4 (a)-(f) ni vitenzi kwa sababu yana irabufupi katika silabi ya pili kutoka mwisho lakini maneno katika mifano 5 (a)-(f) ni nomino baada ya irabundefu kutokea katika mazingira ya irabufupi. Aidha, utofauti wa namna hii hudhihirika kimamatamshi wala si katika maandishi. Aidha, kwa kutumia Nadharia ya KI utofauti wa irabu hizo hudhihirishwa kama ifuatavyo:



Mfano 6 (a) unaonesha irabu katika silabi ya pili kutoka mwisho /u/ ni irabufupi lakini mfano 6 (b) unaonesha irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /u:/ ni irabundefu. Utotauti huo umesababisha mfano 6 (a) kuwa ni kitenzi na mfano 6 (b) kuwa ni nomino licha ya sehemu za neno zingine kufanana. Kimsingi, irabundefu katika 6 (b) hujitokeza katika matamshi wala siyo maandishi ndiyo maana neno hili limeingizwa katika kamusi kama homonimu (neno lenye umbo sawa lakini maana tofauti).

Aidha, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mifano 5 (a)-(e) yanaendana na mazingira ya utokeaji kiasilia wa irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho yaliyoelezwa na Hyman (2003), Kimizi (2003), Kiraka (2013) na Mashauri (2018). Hata hivyo, katika mfano 5 (f) mazingira ya utokeaji wa irabundefu ni utokeaji wa irabundefu kabla ya mkururo wa nazali na konsonanti nyiningezo.

### **3.2 Ubudilikaji wa Nomino kuwa Kitenzi**

Makala hii imebaini kuwa baadhi ya maneno ya Kiswahili yakiwa na irabufupi huwa ni nomino lakini yakiwa na irabundefu katika mazingira hayohayo ya irabufupi hubadilika kuwa vitenzi. Licha ya kuwa jozi husika ya maneno imetambuliwa na KKS ya 2013 kuwa yapo katika kategoria tofauti lakini utofauti huu haukuhusishwa na utokeaji wa irabundefu na irabufupi katika mojawapo ya jozi ya maneno hayo. Tuangalie baadhi ya mifano ya ubudilikaji wa nomino kuwa kitenzi kutokana na utokeaji wa irabundefu.


7. (a) chacha ['ʃatʃa] (N)  
 (b) chaji ['ʃaʃi] (N)  
 (c) chanja ['ʃanʃa] (N)  
 (d) zama ['zama] (N)  
 (e) ripoti [ri'pɔti] (N)  
 (f) paka ['paka] (N)  
 (g) shuka ['ʃuka] (N)  
 (h) pamba ['pamba] (N)  
 (i) nyonga ['ɲɔŋga] (N)

Chanzo: TUKI (2013)


8. (a) chacha ['ʃa:ʃa] (T)  
 (b) chaji ['ʃa:ʃi] (T)  
 (c) chanja ['ʃa:nʃa] (T)  
 (d) zama ['za:ma] (T)  
 (e) ripoti [ri'pɔ:ti] (T)  
 (f) paka ['pa:ka] (T)  
 (g) shuka ['ʃu:ka] (T)  
 (h) pamba ['pa:mba] (T)  
 (i) nyonga ['ɲɔ:n̩ga] (T)

Katika mifano 7 (a)-(i) hapana shaka kuwa maneno hayo ni nomino kwa kuwa matamshi yake huhusisha irabufupi katika silabi ya pili kutoka mwisho lakini katika mifano 8 (a)-(i) maneno hayo ni vitenzi kwa sababu matamshi yake huhusisha irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho. Aidha, tunaweza kudhihirisha utofauti wa wakaa katika irabu hizo kwa kutumia Nadharia ya KI kama ifuatavyo:

9 (a)



9 (b)



Katika mfano 9 (a) irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /a/ ni irabufupi na neno hilo ni nomino lakini katika mfano 9 (b) irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /a/ ni irandefu na neno hilo ni kitenzi. Kwa hiyo, utofauti wa wakaa katika irabu hizi ndiyo una uamilifu wa kubadili kategoria katika maneno haya.

Aidha, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mifano wa 8 (a)-(g) yanaendana na mazingira ya utokeaji kiasilia wa irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho yaliyoelezwa na Hyman (2003), Kimizi (2003), Stegen (2005), Kiraka (2013) na Mashauri (2018). Vilevile, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mfano 8 (h) na (i) yanaendana na mazingira ya utokeaji wa irabundefu kabla ya mkururo wa nazali na konsonanti nyinginezo.


### 3.3 Ubadilikaji wa Nomino kuwa Kibainishi au Kivumishi

Utokeaji wa irabundefu katika mazingira ya irabufupi huweza kusababisha nomino kubadilika kuwa kivumishi au kibainishi. Aidha, irabu hizi hubainika katika matamshi wala si katika maandishi. Kwa hiyo, tukikutana na maneno ya namna hii kwenye matini yanaweza kututatiza lakini utokeaji wa pamoja na maneno mengine ndiyo huweza katuongoza katika utamkaji wa maneno haya. Kwa hiyo, makala hii imebaini baadhi ya maneno yakiwa na irabufupi huwa ni nomino lakini irabundefu

inapotokea katika mazingira hayo ya irabufupi basi neno hilo huwa kivumishi au kibainishi<sup>6</sup>. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

- |                           |                             |
|---------------------------|-----------------------------|
| 9. (a) laini [la'ini] (N) | 10. (a) laini [la'i:ni] (V) |
| (b) changu ['ʃangu] (N)   | (b) changu ['ʃa:ngu] (B)    |
| (c) chungu ['ʃfungu] (N)  | (c) chungu ['ʃu:ngu] (V)    |
| (d) wake ['wake] (N)      | (d) wake ['wa:ke] (B)       |
- Chanzo: TUKI (2013)

Katika mifano 9 (a)–(d) inabainika kuwa utokeaji wa irabufupi katika silabi ya pili kutoka mwisho unasababisha maneno hayo kutamkwa kama nomino lakini katika mifano 10 (a) na (c) utokeaji wa irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho unasababisha maneno hayo kutamkwa kama vivumishi. Vilevile, katika mifano 10 (b) na (d) kuwapo kwa irabundefu kumesababishwa na maneno hayo kutamkwa kama vibainishi. Aidha, tunaweza kudhihirisha utofauti wa wakaa katika irabu hizo kwa kutumia Nadharia ya KI kama ifuatavyo:



Tukirejea mfano 11 (a) irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /a/ ni irabufupi na kategoria ya neno hilo ni nomino lakini katika mfano 11 (b) irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /a:/ ni irabundefu na kategoria ya neno hilo ni kibainishi. Kwa hiyo, utofauti wa kikategoria wa maneno haya huamuliwa na irabundefu katika mfano 11(b).

Aidha, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mfano 10 (a) na (d) yanaendana na mazingira ya utokeaji kiasilia wa irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho yaliyoelezwa na Hyman (2003), Kimizi (2003), Stegen (2005), Kiraka (2013) na Mashauri (2018). Vilevile, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mfano 10 (b) na (c) yanaendana na mazingira ya utokeaji wa irabundefu kabla ya mkururo wa nazali na konsonanti nyinginezo.

### 3.4 Ubadiilikaji wa Kiunganishi kuwa Nomino

Utokeaji wa irabundefu katika mazingira ya irabufupi katika baadhi ya viunganishi husababisha ubadiilikaji wa kategoria kutoka kiunganishi kuwa nomino. Aidha, KKS ya 2013 imeonesha kuwa baadhi ya maneno haya ni homonimu licha ya kuwa na

<sup>6</sup> Kivumishi ni neno linalotokea baada ya nomino au kiwakilishi kuonyesha sifa ya nomino au kiwakilishi husika. Aidha, kibainishi ni neno linalotumika pamoja na nomino au kiwakilishi kuonyesha umahususi wa nomino au kiwakilishi husika (Ndumiwe, 2020).


kategoria na maana tofauti. Makala hii imebaini kuwa utofauti wa kategoria katika maneno ya namna hii hutokana na kutofautiana kwa wakaa katika mojawapo ya irabu za maneno hayo kama inavyodhihirika katika mifano 12 (a) na (b) na 13 (a) na (b).

12. (a) pasi ['pasi] (U)  
 (b) basi ['basi] (U)

13. (a) pasi ['pa:si] (N)  
 (b) basi ['ba:si] (N)

**Chanzo:** TUKI (2013)

Katika mfano 12 (a) na (b) hapana shaka kuwa neno hilo linapotamkwa likiwa na irabufupi katika silabi ya pili kutoka mwisho ni kiunganishi lakini neno hilo hilo linapotamkwa likiwa na irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho kama ilivyo katika 13 (a) na (b) ni nomino. Aidha, kwa kutumia Nadharia ya KI utofauti wa wakaa katika irabu hizo unadhihirishwa ifuatavyo:



Tukirejea mfano 14 (a) irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /a/ ni irabufupi na kategoria ya neno hilo ni kiunganishi lakini katika mfano 14 (b) irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho /a:/ ni irabundefu na kategoria ya neno hilo ni nomino. Kwa hiyo, utofauti wa kikategoria wa maneno haya huamuliwa na irabundefu katika mfano 14 (b).

Hata hivyo, mifano 4 (a)-(f), 7 (a)-(i), 9 (a)-(d) na 12 (a) na (b) inatuthibitishia kuwa si kila neno la Kiswahili lazima liwe na irabundefu. Hii ni kwa sababu irabu zinazotokea katika mifano hiyo ni irabufupi kwa asili yake. Tofauti na mawazo ya akina Hyman (2003), Kiraka (2013), Mashauri (2018) na Ndumiwe (2019) wanaodai kuwa irabu yenye mkazo msingi hurefushwa katika lugha ya Kiswahili. Kimsingi, maneno katika 4 (a)-(f), 7 (a)-(i), 9 (a)-(d) na 12 (a) na (b) yana mkazo msingi katika silabi ya pili kutoka mwisho lakini hayana irabundefu. Kwa hiyo, utafiti zaidi unahitajika kubaini ruwaza za utokeaji wa irabufupi na irabundefu katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, katika KKS ya 2013 kuna baadhi ya vidahizo vinavyotofautishwa kikategoria na irab undefu au irabufupi vimeingizwa kama vidahizo viwili tofauti wala siyo homonimu. Katika vidahizo vyenye irabundefu, irabu hizo hutamkwa kama mwendelezo irabu katika silabi ileile (Stegen, 2005 na Kiraka, 2013). Mifano ifuatayo inadhihirisha haya:

- |                             |                             |
|-----------------------------|-----------------------------|
| 15. (a) nyoka ['njɔ:ka] (N) | 16. (a) nyooka['njɔ:ka] (T) |
| (b) poza ['po:za] (N)       | (b) pooza ['po:za] (T)      |
| (c) pumba ['pumba] (N)      | (c) pumbaa ['pumba:] (T)    |
| (d) shanga ['ʃanga] (N)     | (d) shangaa ['ʃanga:] (T)   |

**Chanzo:** TUKI (2013)

Maneno katika mifano 15 (a)-(d) yana irabufupi katika silabi zake zote lakini maneno katika mifano 16 (a)-(d) yana irabundefu katika mojawapo ya vijenzi vyake. Isitoshe, irabu hizo katika 16 (a)-(d) zimeoneshwa katika othografia ya maneno hayo na hutamkwa kama mwendelezo wala siyo kama irabu inayojirudia. Zaidi ya hayo, maneno hayo yameingizwa kama vidahizo vinavyotofautiana. Walakini, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mfano 16 (a) na (b) yanaendana na mazingira ya utokeaji kiasilia wa irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho yaliyoelezwa na Hyman (2003), Kimizi (2003), Stegen (2005), Kiraka (2013) na Mashauri (2018). Lakini, mazingira ya utokeaji wa irabundefu katika mfano 16 (c) na (d) hayaendani na mazingira yaliyoelezwa hapo awali.

Kwa maoni yetu, data iliyopo katika mfano 4 (a)-(f) na 5 (a)-(f), 7 (a)-(i) na 8 (a)-(i), 9 (a)-(d) na 10 (a)-(d) na 12 (a)-(b) na 13 (a)-(b) inapaswa kuingizwa katika kamusi kama vidahizo viwili tofauti wala siyo homonimu (kama ilivyo kwa sasa) kwa sababu kuwapo kwa irabundefu kunavifanya vitofautiane kama ilivyo katika mifano 15 (a)-(d) na 16 (a)-(d). Suala hili linathibitishwa na Batibo (2002) anayeeleza kuwa maneno mengi yenye jazi pambanuzi finyu yanajitofautisha kutokana na uzito wa silabi, yaani neno lenye irabufupi huwa na uzito wa mora moja ilhali neno lenye irabundefu huwa na uzito wa mora mbili katika kilele cha silabi hiyo. Hata hivyo, katika KKS ya 2013 kuna vidahizo vyenye irabundefu na irabufupi vilivyoingizwa kama vidahizo tofauti. Suala hili tunakubaliana nalo kwa sababu irabu hizo huunda kategoria mbili tofauti lakini tukichunguza kwa umakini tunabaini kuwa hazina irabundefu bali ni irabupacha<sup>7</sup>. Mifano 17 (a)-(e) na 18 (a)-(e) inadhihirisha maelezo haya.

- |                           |                              |
|---------------------------|------------------------------|
| 17. (a) mtala [mtala] (N) | 18. (a) mtaala [m'ta:la] (N) |
| (b) mchuzi [m'ʃuzi] (N)   | (b) mchuuzi [m'ʃu:zi] (N)    |
| (c) mabara [ma'bara] (N)  | (c) maabara [ma:'bara] (N)   |
| (d) madamu [ma'damu] (N)  | (d) maadamu [ma:'damu] (N)   |
| (e) madili [ma'dili] (N)  | (e) maadili [ma:'dili] (N)   |

**Chanzo:** TUKI (2013)

Katika mfano wa 17 (a)-(e) vidahizo tajwa vina irabufupi na vinabainishwa kuwa ni nomino lakini vidahizo katika mifano 18 (a)-(e) vina irabupacha wala siyo irabundefu na vimebainishwa kuwa ni nomino japokuwa vidahizo hivyo

---

<sup>7</sup> Irabupacha ni mfuatano wa irabu mbili zinazofanana katika neno lakini kila moja ina uamilifu wake (Massamba, 2016).

vinatofautiana. Kwa hiyo, utokeaji wa irabupacha katika neno hauwezi kubadili kategoria kama ilivyo kwa irabundefu.

#### **4.0 Athari za Irabundefu kwenye Maana za Maneno**

Kiraka (2013) anaeleza kuwa tofauti ya wakaa wa irabu fulani katika neno inaweza kubadili maana ya neno hilo. Mtaalamu huyu anasisitiza kuwa katika Kiswahili sanifu kuna maneno mengi yaliyo katika jazi pambanuzi finyu ambayo tofauti za maana katika maneno ya jazi hizo hutokana na urefu wa irabu katika mojawapo ya silabi za neno hilo. Hata hivyo, Hyman (2003) anaeleza kuwa lugha nyingi za Kibantu za Mashariki na Kusini zimepoteza sifa ya kutofautisha maana za maneno kwa kutumia urefu wa irabu. Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha hizo zilizozungumziwa na Hyman (2003). Lakini uhalisia unaonesha kuwa katika lugha ya Kiswahili urefushaji wa irabu huweza kutokea katika irabu mojawapo ya maneno yenye jazi pambanuzi finyu na kutofautisha maana za maneno hayo. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili siyo lugha mojawapo iliypoteza sifa ya kutofautisha maana ya neno kwa kutumia irabundefu. Katika Jedwali Na. 1 tumeonesha jinsi utokeaji wa irabundefu katika mojawapo ya maneno yenye jazi pambanuzi finyu yanavyotofautisha maana za maneno hayo.

**Jedwali Na. 1: Maana za Vidahizo vya KKS 3**

<b>Kidahizo kikiwa na Irabufupi</b>		<b>Kidahizo kikiwa na Irabundefu</b>	
<b>Kidahizo</b>	<b>Maana</b>	<b>Kidahizo</b>	<b>Maana</b>
Chanja (N) ['ʃanJa]	Uchaga wa miti unaotumika kuwekea vyombo baada ya kuoshwa.	Chanja (T) ['ʃa:nJa]	Pasua gogo au kuni kupata vipandevipande.
Changa(V) ['ʃanga]	Tunda ambalo halijakomaa.	Changa (T) ['ʃa:nga]	Toa kitu au fedha ili kukusanya kwa makusudi fulani.
Tupa (T) ['tupa]	Peleka au weka kitu kisichohitajika.	Tupa (N) ['tu:pa]	Chombo cha chuma kinachotumika kunolea.
Chuma (T) ['ʃuma]	Toa majani au tunda kutoka kwenye mmea.	Chuma (N) ['ʃu:ma]	Aina ya madini yanayotumika katika ujenzi au utengenezaji wa vitu.
Zama (N) ['zama]	Awamu au wakati fulani.	Zama (T) ['za:ma]	Ingia ndani ya maji kwenda chini.
Ripoti (N) [ri'poti]	Maelezo juu ya mtu, kitu au tukio.	Ripoti (T) [ri'po:ti]	Toa maelezo juu ya mtu, kitu au tukio.
Pamba (N) ['pamba]	Sufi ya mmea iliyoyeupi inayotumika kutengeneza nguo.	Pamba (T) ['pa:mba]	Tayarisha au panga vitu kwa uzuri.
Paka (N) ['paka]	Mnyama mdogo jamii ya chui anayefugwa nyumbani na hupenda kula panya.	Paka (T) ['pa:ka]	Eneza kitu cha majimaji juu ya kitu kingine.
Chungu (N) ['ʃfungu]	Chombo cha kupikia mithili ya sufuria kilichotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi.	Chungu (V) ['ʃu:ngu]	Kinyume cha tamu.
Pasi (U)	Bila ya kuwa; pasipo.	Pasi (N)	Chombo cha chuma kinachotumika

['pasi]		['pa:si]	kunyoshea nguo pindi kipatapo joto.
Changu (N) ['ʃangu]	Samaki wa kijivu mwenye magamba anayepatikana katika majichumvi.	Changu(B) ['ʃa:ngu]	Kibainishi kimilikishi cha nafsi ya kwanza umoja ngeli ya 7.
Laini (N) [la'ini]	Kadi ndogo ndani ya simu inayohifadhi taarifa za mmiliki wa simu hiyo.	Laini (V) [la'i:ni]	Isiyo kwaruza; isiyo ngumu.
wake (N) ['wake]	Wingi wa neno mke.	wake (B) ['wa:ke]	Kibainishi kimilikishi cha nafsi ya pili umoja ngeli ya 1.

**Chanzo:** TUKI (2013)

Maana za vidahizo vya upande wa kushoto na kulia katika Jedwali Na. 1 zinatofautiana. Aidha, utofauti huu unahusishwa na kuwapo kwa irabundefu mwishoni mwa silabi ya pili kutoka mwisho katika vidahizo vya upande wa kulia. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa tofauti ya wakaa katika maneno yenye jozi pambanuzi finyu hubadili maana ya maneno hayo kama alivyodai Kiraka (2013).

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imepambanua athari za utokeaji wa irabundefu katika maana na uainishaji wa maneno ya Kiswahili kwenye KKS 3. Vidahizo vilivyoingizwa ni vile vyenye jozi pambanuzi finyu. Kwa hiyo, baadhi ya maneno yakiwa na irabufupi huwa yanakuwa ya kategoria fulani lakini yanapokuwa na irabundefu katika mazingira ya irabufupi hubadilika kuwa ya kategoria nyingine. Aidha, irabundefu inayosababisha athari katika maana na uainishaji wa maneno hutokea katika silabi ya pili kutoka mwisho. Sanjari na hayo, makala hii imependekeza maeneo mbalimbali yanayohitaji utafiti zaidi kufanyika. Mathalani, baadhi ya vidahizo vilivyoingizwa kama homonimu vimebainika kuwa na maana tofauti na aina tofauti. Kwa mfano, neno “ripoti” [ri'pɔti] likiwa na irabufupi katika silabi ya pili kutoka mwisho ni nomino yenye maana ya *maelezo juu ya mtu, kitu au tukio* lakini likiwa na irabundefu katika silabi ya pili kutoka mwisho [ri'pɔ:ti] ni kitenzi chenye maana ya *toa maelezo juu ya mtu, kitu au tukio*. Kwa mtazamo wetu maneno ya namna hii ni maneno mawili yanayotofautiana. Kwa hiyo, yanapaswa kuingizwa pwekepweke katika kamusi wala siyo homonimu. Hivyo basi, utafiti mwingle unaweza kufanyika kuchunguza kukidhi kwa vidahizo vilivyoingizwa kama homonimu katika KKS3. Hii ni kwa sababu kuwapo kwa irabundefu kunaondoa sifa ya kuwa homonimu bali huwa vidahizo viwili tofauti ukizingatia matamshi.

Vilevile, imebainika kuwa yapo maneno yenye jozi pambanuzi finyu yaliyoingizwa katika KKS 3 kama homonimu lakini hayana irabundefu katika mojawapo ya jozi pambanuzi finyu. Pia, maana na aina za maneno hayo hutofautiana kama ilivyo kwa maneno yenye irabundefu katika mojawapo ya jozi pambanuzi finyu. Kutokana na hilo, makala hii imependekeza utafiti mwingle kufanyika ili

kubaini sababu za mabadiliko ya kikategoría na utofauti wa maana katika maneno ya jazi pambanuzi finyu yenyé irabufupi katika jazi mojawapo.

### Marejeleo

- Batibo, H.M. (2002) "The Evolution of Kiswahili Syllable Structure". *South African Journal of African Language*, 22: 1-10.
- Choge, S. (2009) "Understanding Kiswahili Vowels". *The Journal of Pan African Studies*, 2 (8): 62-77.
- Clements, G. na Keyser, S.J. (1983) *CV Phonology: A Generative Theory of the Syllable*. Cambridge: The MIT Press.
- Hyman, I.M. (2003) Segmental Phonology. Katika D. Nurse na G. Philipson (Wah.) *The Bantu Languages*, 42-58. London: Loutledge.
- Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., Msanjila, Y.P. (2012) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kimizi, M.M. (2003) The Syllable Structure in Standard Swahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kiraka, P. (2013) Urefu, Urefushaji na Ufupishaji wa Irabu katika Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mashauri, M.A (2018) Mwingiliano wa Mashartizuizi ya Viwango vya Sarufi katika Uzalishaji wa Nomino Ambatani katika Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B. (2016) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (Toleo la 2). Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B, Kihore, Y.M na Msanjila, Y.P. (2004) *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B. (2005) "The Role of Suprasegmental Phenomena in the Analysis of Bantu Languages with Special Reference to Ciruuri". *Ocassional Papers in Linguistic, Languages of Tanzania Project*, 1:98-113.
- Massamba, D.P.B. (2011) *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI
- Mgalla, R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longman.
- Ndumiwe, E.J. (2019) Mabadiliko ya Kifonolojia katika Nomino za Kiswahili Zilizotoholewa kutoka Lugha ya Kiingereza: Mifano kutoka *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili* (TUKI, 2006) na *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (Massamba, 2016). Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- \_\_\_\_\_(2020) *Kurunzi ya Isimu na Muundo wa Kiswahili*. Mwanza. Tridax Africa Company Limited.
- Polome, E.C. (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Center of Applied Linguistics.

- Stegen, O. (2005) “Vowel Length in Eastern Bantu Orthographies”. Makala Imewasilishwa katika Kogamano la SIL Bantu Orthograph Lililofanyika Dallas, Novemba 7-12, 2015.
- TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.